SERIKALI YA MAPINDUZI YA
ZANZIBAR

# SERA YA ELIMU ZANZIBAR

WIZARA YA ELIMU ZANZIBAR
Aprili, 1991

## YALIYOMO

| | | Ukura |
|---|---|---|
| **SURA YA KWANZA:** | MAELEZO YA UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 | UMUHIMU WA ELIMU | 1 |
| 1.2 | ELIMU INAYOLENGWA | 2 |
| 1.3 | SHUKRANI | 4 |
| **SURA YA PILI:** | | |
| SERA YA ELIMU, ZANZIBAR | | 6 |
| 2.1 | MAAMUZI MAKUU | 6 |
| 2.2 | MFUMO WA ELIMU | 7 |
| 2.3 | MPANGO WA ELIMU NA AMALI | 8 |
| 2.4 | ELIMU KWA WALEMAVU | 9 |
| 2.5 | USHIRIKIANO NA VYOMBO VISIVYOKUA VYA KISERIKALI KATIKA HUDUMA ZA ELIMU | 9 |
| 2.6 | MUUNDO WA UTUMISHI WA WALIMU | 10 |
| 2.7 | UBORA WA ELIMU | 1 |
| 2.8 | UTEKELEZAJI | 11 |
| **SURA YA TATU:** | | |
| MTU ANAEKUSUDIWA KUANDALIWA KATIKA ELIMU | | 13 |
| **SURA YA NNE:** | | |
| MADHUMUNI NA MALENGO YA ELIMU KWA NGAZI MBALI MBALI | | 15 |
| 4.1 | NGAZI ZA MFUMO WA ELIMU | 15 |
| 4.2 | ELIMU YA MSINGI | 15 |
| 4.3 | ELIMU YA SEKONDARI YA AWALI | 16 |
| 4.4 | ELIMU YA FURSA | 17 |
| 4.5 | ELIMU YA ULEZI | 17 |
| 4.6 | ELIMU YA MAANDALIZI | 18 |
| 4.7 | ELIMU YA SEKONDARI YA PILI | 19 |
| 4.7.1 | Sekondari Ya Michepuo | 19 |
| 4.7.2 | Sekondari Ya Jumla | 19 |
| 4.8 | ELIMU YA SEKONDARI YA JUU | 20 |
| 4.8.1 | Sekondari Ya Juu Ya Michepuo | 20 |
| 4.8.2 | Sekondari Ya Juu Ya Jumla | 21 |
| 4.9 | ELIMU YA WALEMAVU | 21 |
| 4.10 | ELIMU YA WATU WAZIMA | 22 |
| 4.11 | ELIMU YA KUJIENDELEZA | 23 |
| 4.12 | ELIMU YA UALIMU | 23 |

**SURA YA TANO:**
MITAALA YA ELIMU
5.1 MAANA YA MITAALA
5.2 UKUZAJI WA MITAALA NA UTAFITI WA ELIMU
5.3 MITAALA YA ELIMU KATIKA NGAZI MBALI IMBALI
5.3.1 Elimu Ya Maandalizi
5.3.2 Elimu Ya Msingi
5.3.3 Elimu Ya Sekondari Ya Awali
5.3.4 Sekondari Za Pili Na Ju
5.3.5 Mpango Wa Elimu Na Amali
5.3.6 Elimu Ya Ualimu Wa Ulezi/Maandalizi
5.3.7 Elimu Ya Ualimu Wa Msingi Na Sekondari Ya Awali
5.3.8 Elimu Ya Ualimu Wa Sekondari Za Pili Na Juu
5.3.9 Walimu Wengine
5.4. MITAALA YA ELIMU YA WATU WAZIMA
5.4.1 Kusoma, Kuandika Na Kuhesabu
5.4.2 Kisomo Cha Kujiendeleza
5.4.3 Mafunzo Ya Amali
5.5 LUGHA ZA KUFUNDISHA NA KUFUNDISHIA
5.5.1 Lugha Zitazofundishwa
5.5.2 Lugha Za Kufundishia
5.6 - UKAGUZI WA ELIMU
Maslahi Ya Mkaguzi
**SURA YA SITA:**
**WALIMU**
6.1 MAANDALIZI YA WALIMU
6.1.1 Elimu Ya Msingi
6.1.2 Elimui Ya Sekondari
6.2 WAJIBU, HAKI, HUDUMA NA MASLAHI KWA WALIMU
6.2.1 Wajibu Wa Walimu
6.2.2. Haki Za Walimu
6.2.3 Maslahi Ya Walimu
6.2.4 Namna Ya Kuingia Na Kupanda/Kwa Walimu
6.2.5 Walimu Waandamizi
6.2.6 Huduma Maalumu Kwa Walimu
6.2.7 Mafunzo Ya Uongozi Wa Elimu

**SURA YA SABA:**


| | | |
|---|---|---|
| UONGOZI WA ELIMU | | 42 |
| 7.1 | WIZARA NA VIONGOZI WA ELIMU | 42 |
| 7.2 | UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU | 42 |
| 7.2.1 | Viongozi Wa Ngazi Za Juu | 42 |
| 7.2.2 | Viongozi Wa Ngazi Za Kati | 42 |
| 7.2.3 | Viongozi Wa Ngazi Za Chini | 43 |
| 7.2.4 | Viongozi WA Muda | 43 |
| 7.3 | MUUNDO WA UONGOZI WA ELIMU | 43 |
| 7.4 | WAJIBU WA WIZARA YA ELIMU | 43 |
| 7.5 | AFISI ZA ELIMU ZA MKOA NA WILAYA | 44 |
| 7.6 | SKULI NA WAJIBU WAKE | 44 |


**SURA YA NANE:**


| | | |
|---|---|---|
| VYOMBO VYENGINE VYA ELIMU | | 46 |
| 8.1 | VYOMBO NA TAASISI ZA ELIMU | 46 |
| 8.2 | TAASISI YA LUGHA | 46 |
| 8.3 | MAKTABA | 46 |
| 8.4 | MAKTABA KUU | 47 |
| 8.5 | MAKTABA ZA WILAYA | 47 |
| 8.6 | MAKTABA ZA SKULI | 47 |
| 8.7. | TUME YA UTUMISHI WA WALIMU | 48 |
| 8.8 | TAASISI ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI | 48 |


**SURA YA TISA:**


| | | |
|---|---|---|
| MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA ŞERA HII | | 49 |
| 9.1 | MALIPO YA USAFIRI KWA WANAFUNZI | 49 |
| 9.2 | BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA TANZANIA | 49 |
| 9.3 | ELIMU KWA NJIA YA VYOMBO VYA HABARI | 49 |
| 9.4 | MCHANGO WA WANANCHI KATIKA GHARAMA ZA ELIMU | 50 |
| 9.5 | UTHIBITISHO WA VYETI VYA MASOMO | 50 |
| 9.6 | HATUA ZA UTEKELEZAJI | 51 |


**SURA YA KUMI:**


| | |
|---|---|
| MWISHO | 52 |
| NYARAKA ZILIOTUMIKA KUTAYARISHA SERA | 53 |

# SURA YA KWANZA

## 1.0. MAELEZO YA UTANGULIZI

### 1.1. UMUHIMU WA ELIMU

1.1.1. Elimu ni nyenzo muhimu na ya msingi inayomwezesha mwanadamu kuyasanifu mazingira kwa manufaa yake. Kuna makubaliano ya jumla ya kimataifa kwamba elimu ni mojawapo ya haki za binaadamu. Hata hivyo utoaji wake popote pale duniani unategemea mwelekeo wa kiitikadi na kisiasa wa nchi. Kila taifa huweka malengo yake ya msingi ambayo hulingana na falsafa ya utawala wa taifa hilo, hali ya wakati na mahitaji ya taifa kwa wakati huo au kwa kipindi maalum kinachotazamiwa. Aidha, malengo hayo ya elimu hutegemea maendeleo mengine ya kiuchumi na kijamii yanayobuniwa na kupangwa na taifa.

1.1.2. Ingawa malengo hayo ya elimu huwa mahsusi kwa taifa linalohusika, hapana taifa lolote duniani linaloishi au linaloweza kuishi peke yake. Kila taifa linaishi katika jamii ya mataifa mengine na bila shaka taifa moja huweza kuliathiri taifa jengine kwa namna moja au nyingine. Uzoefu unaonesha kwamba mataifa yaliyoendelea ndiyo yanayoyaathiri zaidi, ama kwa uzuri au kwa ubaya, mataifa machanga kama hili letu. Hayo hutokea kutokana na historia ya kutawaliwa na kwa kuiga mifumo ya mataifa yaliyoendelea na kudhani kwamba huko ndiko kuendelea.

1.1.3. Kwa kuwa elimu ni nyenzo ya jamii na kwa sababu jamii ndiyo inayoathirika, ni dhahiri kwamba ili elimu yoyote inayotolewa iwe ya manufaa kwa jamii ni lazima ikubaliane na falsafa ya jamii inayohusika, jamii hiyo ishiriki kikamilifu katika upangaji, utoaji, usimamiaji na ufanyaji wa tathmini ya elimu hiyo. Hayo yote hufanywa na jamii kwa madhumuni ya kuendeleza malengo ya kukidhi maadili na falsafa za kisiasa, na

kukuza mila na utamaduni wa taifa.

1.1.4. Jamii pia hutumia elimu kuwa ni nyenzo ya kuvirithisha vizazi vyake yale ambayo jamii imeyaona ni bora yaendelezwe na kuyakataza yale ambayo jamii imeyaona hayafai. Kwa hali hii elimu na malengo yake lazima yawe hai kukabili, kuchangia na kupokea mabadiliko yanayoletwa na maendeleo. Kama elimu na malengo yake yatakwama katika kukubali kuchangia mabadiliko, itakuwa ni kikwazo kikubwa cha kuleta maendeleo ya jamii.

1.1.5. Mbali na kupanga hayo, elimu huhitajia kuwepo kwa mbinu na ufundi wa kuyafikia malengo hayo yaliyopangwa na jamii. Malengo hayo ni vyombo hai vinavyokua, kubadilika, kufa na kutoweka. Mbinu na ufundi mpya wa kufikia malengo ya elimu ni njia za maendeleo zinazokua kwa kasi. Jamii lazima ielewe kuwa kung'ang'ania mbinu na njia zilizopita kwa upande mmoja au kuzikataa na kuzikejeli kwa kuwa ni za kizamani kwa upande mwengine bila ya kuzichunguza vyema, huweza kuwaviza vijana wetu wasiweze kupata maendeleo kulingana na mabadiliko ya haraka ya ulimwengu wa leo.

## 1.2. ELIMU INAYOLENGWA

1.2.1. Elimu hupatikana kwa juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na jamii ili kuiwezesha jamii yenyewe kuuelewa ulimwengu kwa undani zaidi na pia kupata maarifa, ujuzi na ufundi au stadi za kudumisha uhai wa jamii na kukuza utu wenye sifa zote zinazothaminiwa na jamii hiyo.

1.2.2. Kwa hivyo lengo la elimu si kuiongezea jamii kiasi cha maarifa tu, lakini pia kuwa na uwezo wa kujiendeleza katika kuvumbua, kugundua na kuunda vitu, mbinu na tabia zitakazoweza kuisaidia jamii kuyamudu vizuri na kwa raha mazingira yanayoizunguka jamii hiyo.

1.2.3. Ugumu wa kuweka na kubuni malengo ya elimu unazidi kadri jamii inavyobadilika kutokana na maendeleo ya haraka ya sayansi, teknolojia na taaluma nyinginezo. Pia, taathira za mabadiliko yanayoletwa kwa kuingia mila na tamaduni za kigeni zinapunguza uwezo wa kutabiri kwa matayarisho ya vijana waliopo sasa na ambao wanatarajia kuishi kikamilifu hivi sasa na miaka ijayo. Lakini wajibu wa kuwa na m alengo na mbinu za utekelezaji kutokana na mahitaji ya jamii, unazidi uzito wa kikwazo chochote kile. Muhimu zaidi la kuzingatiwa kila mara ni kwamba ukuaji wa elimu ni kitu chenye uhai, yaani elimu hukua na kubadilika.

1.2.4. Kwa kuwa tunaelewa wazi kwamba jamii ya Zanzibar pamoja na Serikali yake inaongozwa na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, na falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inayotokana na Azimio la Arusha, Sera ya Elimu ya Zanzibar haina budi kutafsiri kwa mawazo na vitendo azma na malengo ya siasa na falsafa hizo kwa kuzingatia historia, watu na mahitaji ya Zanzibar.

1.2.5. Kwa hivyo lengo kuu la elimu Zanzibar ni kumpa fursa kila Mzanzibari ajitokeze kutumia vipaji vyake vyote na pia kumjenga katika maadili ya Ujamaa na Kujitegemea. Ili kufikia lengo hilo tunahitaji kwanza, miongoni mwa mambo mengine, sera sahihi ya elimu inayolenga kwenye Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ikifuatiliwa na haya yafuatayo:-

1.2.5.1. Miongozo na mitaala mwafaka kwa mujibu wa azma ya elimu.

1.2.5.2. Vifaa vya kutosha katika ngazi na aina zote za elimu.

1.2.5.3. Walimu wa kutosha walioandaliwa vilivyo na kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika.

1.2.5.4. Madarasa na samani zinazostahiki.

1.2.5.5. Nyenzo kama vile maabara, karakhana na mashamba ya kilimo.

1.2.5.6. Nyumba za walimu (hasa mashamba) na viwanja vya michezo kwa ajili ya skuli

1.2.5.7. Utafiti wa kitaalamu pamoja na tathmini ya elimu itolewayo ili kujiimarisha, kujikosoa au hata kujipongeza pale inapostahiki, katika mipango yetu ya elimu.

1.2.5.8. Usimamiaji imara na utekelezaji wa Sera yenyewe ili ufanisi upatikane.

1.2.5.9. Vyombo vya usafiri vitavyowezesha maafisa kama vile Maafisa Elimu wa Wilaya, Mikoa na Wakaguzi kuweza kufuatilia usomeshaji na kazi za kujitegemea.

1.2.5.10. Kwa sababu Sera hii ya Elimu ni ya Taifa inahitaji kusimamiwa na vyombo vingi katika hatua zake zote za utayarishaji wa mpango wa utekelezaji. Hivyo usimamizi na uongozi wa vyombo vifuatavyo utahitajika:-

- Vyama vya Kisiasa.
- Jumuiya za Wananchi
- Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (vyombo vyake vyote na hasa Wizara ya Elimu) Taasisi na vyombo vyengine vya kitaifa na kimataifa.
- Watu wenyewe, yaani wazazi, wanafunzi n.k.

## 1.3. SHUKRANI

1.3.1. Utayarishaji wa Sera hii ya Elimu ya Zanzibar usingelifanikiwa kama si mashirikiano ya watu na vyombo vilivyo nje ya Wizara ya Elimu. Kwa hivyo Wizara ya Elimu inachukua fursa ya kutoa shukran i za dhati kwa watu na vyombo hivyo. Wizara ya Elimu haiwezi kuorodhesha hapa majina na vyombo hivyo vyote lakini shukrani zenyewe hazitokamilika ikiwa miongoni mwa watu waliotajwa; walimu, wanafunzi,

wazee na wataalamu nje na ndani ya nchi hawatatajwa angalau kwa ujumla wao.

1.3.2. Aidha Wizara ya Elimu inatoa shukrani maalum kwa Tume ya Rais ya Elimu, na UNESCO kwa kuruhusu ripoti zao za Elimu kutumika katika utayarishaji wa mapendekezo ya awali ya Sera ya Elimu ya Zanzibar.

1.3.3. Shukrani maalum ziuendee Mkutano wa Dunia juu ya Elimu Kwa Wote ambao ulifanyika Jomtien, Thailand tarehe 5-9 Machi, 1990. Maazimio ya Mkutano huo yalitoa msukumo (inspiration) katika hatua za mwisho za maandalizi ya Sera hii.

1.3.4. Mwisho, shukrani ziiendee Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuibariki na kuipitisha Sera hii.

# SURA YA PILI

## 2.0. SERA YA ELIMU - ZANZIBAR

### 2.1. MAAMUZI MAKUU

2.1.1. Kwa muda mrefu shughuli za Elimu humu Visiwani Zanzibar zimekuwa zikiendeshwa bila ya sera maalum ya utekelezaji inayoeleweka. Inaeleweka kwamba Siasa ya Chama cha Afro-Shirazi mara tu baada ya Mapinduzi ya 1964 ilikuwa ni kutumia huduma ya elimu katika kuleta usawa katika jamii yetu. Ndiyo maana ikaamuliwa kwamba elimu itatolewa kwa wote tena bila ya malipo katika ngazi zote za elimu kuanzia elimu ya msingi hadi viwango vya juu kabisa. Inaeleweka pia kwamba Zanzibar imekua ikijaribu kutekeleza Sera ya Elimu ya Kujitegemea ambayo ni sehemu muhimu ya Azimio la Arusha. Lakini muda wote huo, tumekuwa hatuna dira inayoeleweka ya kutuongoza katika utekelezaji wa sera hiyo.

2.1.2. Kutokana na ukosefu wa sera ya utekelezaji wa elimu nchini, kumelimbikizana matatizo mengi ya kiutekelezaji ambayo yanatufanya tuonekane kama kwamba hatujui twendako. Ndio maana katika mwaka 1982, aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ndugu Aboud Jumbe Mwinyi, aliamua kuunda Tume ya Elimu ambayo iliufanyia tathmini mfumo mzima wa Elimu na kutoa mapendekezo ya mabadiliko mbali mbali. Pia mwaka 1983 Wizara ya Elimu Zanzibar iliomba UNESCO kuisaidia katika kuufanyia tathmini mfumo wetu wa elimu ya sekondari, hasa kuhusu suala la utekelezaji wa elimu ya kujitegemea katika ngazi hii. Kazi hii ilifanywa kwa ufanisi mkubwa sana, na ndipo lilipozaliwa wazo la Mpango wa elimu na Amali (MENA) ambao utakuwa ndiyo kiini cha mtaala mpya wa elimu ya sekondari.

2.1.3. Kwa jumla, Sera hii imejengwa juu ya msingi wa mapendekezo mbali mbali ya Tume ya Rais ya Elimu, yale ya UNESCO na yale ya mkutano wa Dunia juu ya Elimu kwa wote uliofanyika Jomtien, Thailand, mwaka 1990. Sera hii inajaribu kuweka miongozo ya jumla ya utaratibu unaofaa wa utekelezaji wa siasa ya Chama na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juu ya Elimu. Kwa hiyo baadhi ya mambo yaliyotajwa katika sera hii yamekwishaanza kutelekezwa. Mfano ni yale yanayohusu mtaala wa Elimu ya msingi, lakini mengi ni mapya ambayo yanapewa ufafanuzi mkubwa zaidi katika Sera.

Mabadiliko makuu ni kama yafuatayo:-

## 2.2. MFUMO WA ELIMU

2.2.1. Zanzibar itakuwa na mfumo wa 7-3-2-2 badala ya 8-3-1-2. Kwa ufafanuzi zaidi ni:- Elimu ya Msingi - miaka 7. Umri wa kuanza skuli utakuwa miaka 7.

Elimu ya Sekondari ya Awali - miaka 3.

Elimu ya Sekondari ya Pili - miaka 2.

Elimu ya Sekondari ya Juu - miaka 2.

Mfumo wa Elimu baada ya hapo utakuwa wa pamoja na Tanzania Bara.

2.2.2. Kwa mfumo huu, Elimu ya Lazima itakuwa kuanzia Msingi hadi Sekondari ya Awali, yaani miaka 10. Elimu hii itakuwa ni haki ya kila Mzanzibari na itakuwa ni ya lazima kisheria, kwa wote. Jitihada zitafanywa ili elimu hii iwafikie wote wanaostahiki ifikapo mwaka 2000, chini ya msingi wa maamuzi ya Mkutano wa Dunia juu ya Elimu Kwa Wote.

2.2.3. Baada ya kuangalia mifumo ya elimu ya nchi nyingi ulimwenguni imebainika kwamba miaka minane ni mingi sana kwa elimu ya msingi. Nchi nyingi ulimwenguni zinatoa elimu ya msingi ya miaka 5 au 6 tu, lakini kwa upande wetu hapa Zanzibar, hatuwezi kuupunguza muda wa elimu ya msingi kuwa chini ya miaka 7, hasa tukizingatia haja ya watoto wetu kusomeshwa lugha 3 yaani Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu.

2.2.4. Mwaka mmoja umeongezwa katika ngazi ya Sekondari ya Pili ili kupunguza taathira katika kiwango cha elimu ya darasani baada ya kuongezwa kwa msisitizo juu ya mafunzo ya kazi za vitendo chini ya utaratibu wa Mpango wa Elimu na Amali.

## 2.3. MPANGO WA ELIMU NA AMALI

2.3.1. Kutaanzishwa programu ya mafunzo ya vitendo katika sehemu za ngazi ya sekondari, ambayo itajulikana kwa jina la Mpango wa Elimu na Amali (MENA). Programu hii ina lengo kuu la kutafsiri kwa vitendo sera ya Elimu ya Kujitegemea katika ngazi mbali mbali za elimu. Chini ya utaratibu wa MENA wanafunzi wote katika ngazi ya msingi watazowezwa kidogo kidogo kazi mbali mbali za uzalishaji mali na katika ngazi ya sekondari ya awali, watapata mafunzo ya msingi ya ufundi, amali na teknolojia. Katika ngazi ya sekondari ya pili na ya juu, mafunzo yatagawika katika michepuo ya Biashara, Ufundi, Kilimo, Uvuvi, Sayansi ya Nyumbani na mengineyo itakayoonekana inafaa kulingana na wakati.

Aidha vyuo vya elimu vitatoa mafunzo maalum yatakayowawezesha walimu kumudu kufundisha kazi za amali. Wizara ya Elimu haitojishughulisha sana na mafunzo ya ufundi stadi (vocational training) ambayo yatatolewa na sekta mbali mbali zinazohusika, isipokuwa pale ambapo kufanya hivyo, kutasaidia ufanisi wa utekelezaji wa MENA. Uchambuzi wa

ufafanuzi wa MENA utatolewa katika waraka maalum utaoandaliwa. Kuhusu mafunzo ya ufundi stadi nchini, itaandaliwa sera maalum na chombo kinachohusika. Elimu ya kawaida itaendelea kutolewa sambamba na utaratibu wa MENA, ila tu katika ngazi ya Sekondari, nayo itafanyiwa michepuo (specializations) ya Sayansi, Lugha, Sayansi Jamii, na mengineyo itayohitajika.

## 2.4. ELIMU KWA WALEMAVU

Wizara ya Elimu kwa mashirikiano na vyombo vyengine vya Serikali pamoja na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, itahakikisha kwamba haki na fursa za elimu ambazo Serikali inazitoa kwa Wazanzibari wote, pia zitatolewa kwa misingi ile ile kwa walemavu. Ulemavu kwa kadri itavyowezekana hautakuwa kikwazo wala sababu ya kumnyima mwanadamu haki ya elimu. Sera maalum ya utekelezaji wa azma hii, itaandaliwa.

## 5. USHIRIKIANO NA VYOMBO VISIVYOKUWA VYA SERIKALI KATIKA HUDUMA ZA ELIMU

5.1. Kwa mujibu wa Sera hii, Serikali itagharimia tu elimu ya fursa (ile isiyokuwa ya lazima) kwa mujibu wa uwezo wake na mahitaji ya Taifa. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba haitaweza kukidhi mahitaji yote ya jamii juu ya elimu hii, na kwa sababu hiyo, Serikali itaanza kuruhusu kuanzishwa kwa skuli za binafsi zitakazotoa elimu ya fursa ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya elimu ya wananchi wa Tanzania Zanzibar.

Mashirika mbali mbali yakiwa ni pamoja na ya Dini na watu binafsi yataweza kuanzisha skuli hizo, hasa katika nyanja za elimu za ufundi na teknolojia. Masharti yatakayohakikisha kuwa uanzishaji wa skuli za aina hiyo hautakuwa holela na kuwa utazingatia mahitaji ya elimu ya wananchi wa Zanzibar yatawekwa. Aidha, masuala ya viwango vya elimu vitakavyotolewa na skuli

za binafsi, mazingatio ya usawa katika uanzishwaji na uendeshaji wake, na mwelekeo wa kihuduma zaidi kuliko kibiashara, ni miongoni mwa masharti yatayowekwa.

2.5.2. Kwa upande wa elimu ya lazima ambayo itatolewa katika skuli za Serikali chini ya msingi wa elimu bila malipo, Serikali itashawishi michango ya hali na mali ya aina mbali mbali, kutoka kwa wazazi, wananchi kwa jumla na wahisani mbali mbali, kwa lengo la kusaidiana katika kuubeba mzigo huu mzito.

**2.6. MUUNDO WA UTUMISHI WA ELIMU**

2.6.1. Kutokana na jinsi ya kazi ya ualimu inavyotafautiana sana na kazi nyengine katika utumishi Serikalini, patakuwa na muundo maalum wa utumishi, mahsusi kwa mwalimu tu, ikiwa ni pamoja na mishahara na taratibu za upandishaji vyeo. Muundo huu wa mishahara ya walimu utagezewa na mishahara ya Utumishi Serikalini hapa Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa jumla wakati wote itahakikishwa kwamba:-

(a) Kima cha chini cha mishahara ya walimu kinakizidi kima cha chini cha mishashara ya Utumishi Serikalini hapa Zanzibar kwa nyongeza zisizopungua tatu na au

(b) Mishahara (hasa kima kinachobaki baada ya mkato) ya walimu wetu haipitani sana na ile ya walimu wa Tanzania Bara, mradi tu tofauti haitakuwa kubwa sana baina yake na ile ya watumishi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

2.6.2. Ili kukabiliana na kasoro iliyojitokeza huko nyuma ya kutokuwepo kwa mfumo wa utumishi unaozingatia kwa ukamilifu maslahi ya mwalimu na ambao moja kwa moja ungeweza kumpandisha daraja mwalimu akiwa katika kazi yake ya ualimu bila ya kulazimika

kumuondoa katika kazi ya usomeshaji, pataanzishwa vyeo maalum ndani ya 'profession' ya ualimu ambavyo vitakuwa na hadhi sawa na ile ya maafisa mbali mbali wa elimu. Nafasi za vyeo hivyo vitavyojulikana kama Walimu Waandamizi wa ngazi mbali mbali zitakuwa zikitengwa kila mwaka. Aidha cheo cha Mwalimu Mkuu kitapewa hadhi kinayostahiki na kupangiwa mshahara wake maalum. Aidha itaundwa kisheria Tume ya Utumishi wa Walimu ambayo itasimamia ajira, haki, maslahi, huduma na wajibu wa walimu.

**2.7.0. UBORA WA ELIMU**

2.7.1. Pamoja na kuzingatia umuhimu wa kutoa elimu kwa wingi (yaani kwa wote) Sera hii inasisitiza ubora wa hali ya juu wa elimu itolewayo. Kwa hivyo, mipango yote ya maendeleo ya elimu itayoandaliwa itatilia maanani azma hii ya msingi na ambayo imetiliwa mkazo katika azimio la kimataifa la Jomtien kuhusu elimu kwa wote.

**2.8.0. UTEKELEZAJI**

2.8.1. Utaratibu wa utekelezaji wa Sera hii ya elimu utakuwa wa hatua kwa hatua, badala ya kufanya mabadiliko ya ghafla, ili kuhakikisha kwamba utekelezaji huo hauambatani na kushuka kwa kiwango cha elimu. Mabadiliko ya idadi ya miaka ya elimu ya lazima kwa wote kutoka miaka 11 hadi 10 yatakuwa ya mara moja, lakini yale ya kutoka mfumo wa 8-3-1-2 kuingia 7-3-2-2 yatachukua muda mrefu. Katika Kipindi cha Mpito, kutakuwa na mikondo miwili mikuu ya wanafunzi, itayokwenda sambamba.

Mkondo wa Kwanza ni ule utaoingia katika mfumo mpya ambapo watachaguliwa wanafunzi kutoka Darasa la 7 wataoingia katika madarasa ya MENA, na

kuendelea hadi kumaliza Sekondari ya Awali (Darasa la 10).

Mkondo wa Pili utaendelea Darasa la 8 kama ilivyo hivi sasa na baadae kuingia Sekondari Kidato cha 1 na cha 2 (Darasa la 10). Kadri madarasa ya MENA yatavyokuwa yanaongezeka, ndivyo mkondo wa pili (Mfumo Mkongwe) utakavyokuwa unamalizika.

Aidha, kwa jumla, utekelezaji wa Sera hii, utakwenda sambamba na kwa uwiano wa karibu sana na utekelezaji wa Sera ya Malezi ya Taifa kwa Watoto na Vijana Tanzania, na ile ya Mafunzo ya Ufundi Stadi itapofungwa.

# SURA YA TATU

## 3.0. MTU ANAEKUSUDIWA KUANDALIWA KATIKA ELIMU

3.1. Madhumuni na lengo kuu la elimu Zanzibar ni kumtayarisha Mzanzibari atakayeweza kuishi ipasavyo hapa Zanzibar, Tanzania kwa jumla na popote duniani. Kwa hivyo Mzanzibari anayefikiriwa kwa dhana hii ni yule aliyetayarishwa kuwa na sifa kama ifuatavyo:-

3.1.1. Mwenye maarifa ya kutosha na uwezo wa kuyaendeleza maarifa hayo kwa maslahi yake, jamii yake, Zanzibar na Taifa la Tanzania kwa jumla.

3.1.2. Mwenye kutumia maarifa aliyonayo ili kuyasanifu na kuyasarifu mazingira kwa maendeleo yake, jamii yake na Taifa zima.

3.1.3. Mwenye kuyatumia maarifa katika uchunguzi,, na ubunifu wa mbinu za kazi zinazokubalika katika jamii.

3.1.4. Mwenye kupenda kujifunza na kuwafundisha wenzake bila ya ubaguzi wa aina yoyote ile.

3.1.5. Mwenye kupenda na kuthamini kazi ya halali.

3.1.6. Mwenye kubuni, kupanga na kutumia taratibu nzuri za kazi.

3.1.7. Mwenye kupenda kutumia na kutunza vyema zana za kazi.

3.1.8. Mwenye kupenda kushiriki katika kazi zenyewe bila kujali kazi za ziada.

3.1.9. Mwenye moyo wa kujiamini katika kuamua mambo yaliyokubalika chini ya misingi ya kidemokrasia.

3.1.10. Mwenye kupenda kuthamini na kuendeleza uhuru wake, wa wenzake na wa Taifa zima, mradi tu havunji sheria.

3.1.11. Mwenye moyo wa kujitolea katika kuwasaidia wenzake, watoto, watu wazima na jamii yote.

3.1.12. Mwenye kupenda kuthamini, kudumisha na kuendeleza desturi, mila na utamaduni na maadili ya Taifa.

3.1.13. Mwenye kupenda kuheshimu na kuheshimiwa na wadogo zake, wakubwa na watu wengine katika jamii yake.

3.1.14. Mwenye ustahamilivu wa kutoa na kupokea ushauri kwa misingi ya kidemokrasia.

3.1.15. Mwenye kupenda ukweli, haki za binaadamu, wenzake, popote pale ulimwenguni na mwenye kudumisha amani kwa mujibu wa sheria za nchi na za Kimataifa.

3.1.16. Mwenye kutumia lugha nzuri katika mkabala wake na watu wote.

3.1.17. Mwenye kutekeleza kwa vitendo falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea.

3.1.18. Mwenye kudumisha umoja wa Tanzania na kupendelea Umoja wa Afrika nzima.,

3.1.19. Mwenye kutii uongozi, mamlaka na sheria za Zanzibar, Tanzania na za Kimataifa.

3.1.20 Mwenye kuyaelewa matatizo ya nchi na kujenga uzalendo wa kushiriki katika kuyatatua kwa upande mmoja, na mwenye kuyathamini mafanikio ya nchi yanayopatikana kwa upande mwengine.

# SURA YA NNE

## 4.0. MADHUMUNI NA MALENGO YA ELIMU KWA NGAZI MBALI MBALI

### 4.1. NGAZI ZA MFUMO WA ELIMU

4.1.1. Mfumo wa Elimu utakuwa na ngazi mbali mbali kama zilivyooneshwa katika Mchoro "A". Kila ngazi itamtayarisha mwanafunzi ili aweze kubadili maisha yake ipasavyo na kutoa michango yake kwa Taifa. Elimu ya lazima itakuwa ya miaka 10 na itagawika katika ngazi ambazo ni miaka 7 ya Elimu ya Msingi na miaka 3 ya Elimu ya Sekondari ya Awali.

### 4.2. ELIMU YA MSINGI

4.2.0. Vijana wanaoanza maisha ya skuli lazima waongozwe kwenye mwelekeo wa kupenda masomo yao na kuanza kujengwa kwa tabia na mtazamo wa yule anayetayarishwa kama ilivyofafanuliwa katika Sura ya Tatu. Katika kumjenga Mzanzibari huyu, Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ndiyo itakayokuwa dira thabiti ya matendo na mbinu zitazotumika. Kwa hivyo madhumuni ya ngazi hii yatakuwa kama ifuatavyo:-

4.2.1. Kuweka, kuimarisha na kuendeleza misingi imara ya kudumu katika kusoma, kuandika na kuhesabu.

4.2.2. Kuweka, kuimarisha na kuendeleza misingi imara ya kufikiria na kudadisi, kwa lengo la kuelewa mazingira na mahusiano ya kijamii.

4.2.3. Kugundua vipaji vya watoto toka wangali wadogo kwa madhumuni ya kuviendeleza.

4.2.4. Kuwatayarisha watoto kuwa na misingi ya kuchungua, kufikiria, kuchambua na kushirikiana kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayozuwia au kuchelewesha maendeleo yao na ya jamii yao.

4.2.5. Kuwatayarisha watoto kwa ajili ya elimu ya Sekondari ya Awali.

4.2.6. Kuanza kuwatayarisha watoto kwa elimu ya Kujitegemea,kwa kuwazowesha kazi za uzalishaji mali.

4.2.7. Kuwajenga watoto kimaadili, kiutamaduni na kiitikadi kwa kuwapa misingi ya kuielewa nchi yao kihistoria, kimazingira, kisiasa na kijamii.

4.2.8 . Kujenga tabia ya ukakamavu na kupenda usafi miongoni mwa watoto.

**4.3. ELIMU YA SEKONDARI YA AWALI**

4.3.0. Elimu ya Sekondari ya awali ni maendeleo ya Elimu ya Msingi. Elimu ya Sekondari ya Awali italenga kumkamilishia mwanafunzi elimu ya lazima ambayo itampa mafunzo yatakayomsaidia kujitegemea. Kwa hivyo malengo ya ngazi hii ya elimu yatakuwa kama ifuatavyo:-

4.3.1. Kumtayarisha mwanafunzi kwa maisha ya kujitegemea baada ya kumaliza skuli.

4.3.2. Kuendeleza pale Elimu ya Msingi ilipoishia.

4.3.3. Kumuwezesha kuelewa na kutumia mbinu za Sayansi na Teknolojia.

4.3.4. Kumwezesha mwanafunzi kumudu mazingira yake vizuri kwa kumuongoza kufanya kazi za amali na mbinu za kukabiliana na matatizo mbali mbali.

4.3.5. Kumtayarisha mwanafunzi kuendelea na masomo yatakayotolewa baada ya ngazi hii pindipo atapata fursa hiyo.

4.3.6. Kumwekea mwanafunzi misingi ya kuweza kujiendeleza mwenyewe kwa kutumia fursa za elimu ya kujiendeleza (continuing education) zitakazokuwapo.

## 4.4. ELIMU YA FURSA

4.4.1. Elimu ya fursa itatolewa kwa wale wenye sifa zitakiwazo na watakaobahatika kuipata. Kwa sababu hiyo Serikali ya Mapinduzi itaruhusu vyombo mbali mbali kushiriki katika utoaji wa elimu hiyo mradi tu masharti yaliyowekwa au yatayowekwa na sheria ya Elimu na matoleo mbali mbali ya kiserikali, yatatimizwa na wahusika wote, na suala la usawa litazingatiwa. Elimu ya fursa itajumuisha ulezi, Elimu ya Maandalizi na elimu yote baada ya elimu ya lazima.

4.4.2. Pamoja na kuwa elimu hii itakuwa ya fursa, madhumuni yake yanabaki yale yale kama ya elimu ya lazima. Kwa vyo vyote vile, elimu hii haitoachiwa kuvunja misingi ya haki na usawa katika jamii katika utoaji na uendelezaji wake.

## 4.5. ELIMU YA ULEZI

4.5.1. Taaluma kuhusu ukuaji wa akili ya mwanadamu inasisitiza wazi kwamba miaka ya kwanza ya mwanadamu (mtoto) ni miaka yenye umuhimu mkubwa katika kuweka misingi imara. Huu ndio wakati bora wa kujenga utu, maadili, akili na ujuzi wa siku za mbele. Kwa hivyo basi, Serikali itatilia mkazo elimu katika kiwango hicho. Lakini kutokana na uwezo wake mdogo wa kifedha katika kukabili gharama za elimu ya kiwango hiki, Sera hii inaungana na Sera ya Malezi ya Taifa kwa Watoto na Vijana katika kuhimiza wananchi kushughulikia elimu hii wao wenyewe katika maeneo yao wanamoishi, na wanamofanya kazi. Watoto wachanga wenye umri wa baina ya miezi mitatu na miaka 3 ndio watakaohusika.

4.5.2. Vituo vya kulelea watoto hao vitaanzishwa kama itakavyowezekana na kukubaliwa kisheria. Lengo kuu la vituo hivyo litakuwa ni kuwasaidia wazazi kuwatunzia watoto wao kwa vizuri ili waweze kushiriki katika uzalishaji mali bila ya kufungika kwa ulezi wa watoto.Suala hili litasimamiwa na chombo cha Serikali, kinachoshughulikia ustawi wa jamii.

## 4.6. ELIMU YA MAANDALIZI

4.6.1. Ngazi hii ya elimu inawakusudia watoto wa miaka minne mpaka sita (4-6). Vituo vya kutoa Elimu hii vitaenezwa kwa mujibu wa haja na uwezo utavyoruhusu kwa masharti yatakayowekwa. Malengo ya ngazi hii yatakuwa:-

4.6.1.1. Kuwasaidia watoto kukua vizuri kimwili na kiakili kwa kuwapatia mahitaji yanayolingana na umri wao.

4.6.1.2. Kumpa kila mtoto fursa ya kujitambua uwezo wake na kuweza kuutumia uwezo huo kuchangia maendeleo kwa kushirikiana na wenziwe.

4.6.1.3. Kuendeleza na kusaidia malezi ya nyumbani.

4.6.1.4. Kuwalea watoto kwa kuwapa maadili ya Taifa,mila na utamaduni pamoja na mafunzo mengine ya manufaa.

4.6.1.5. Kujaribu kuwatambua watoto wenye maendeleo mazuri ya kiafya na kiakili na wale wenye ulemavu wowote ili waweze kuhudumiwa ipasavyo.

4.6.1.6. Kuwatayarisha watoto kwa Elimu ya Msingi.

## 4.7. ELIMU YA SEKONDARI YA PILI

Ngazi hii ya elimu itakuwa na madhumuni makuu ya kutayarisha wataalamu wa ngazi na aina mbali mbali na itagawika katika sehemu mbili zifuatazo:-

### 4.7.1. Sekondari Ya Michepuo

Serikali itahimiza, itaanzisha na itatilia mkazo zaidi skuli za Sekondari za Michepuo na hasa za ufundi kulingana na mahitaji ya jamii, Michepuo itakayokuwepo italingana na mafunzo ya kazi za amali zitakazofundishwa katika skuli za Sekondari ya Awali. Malengo ya sehemu hii yatakua kama hivi:

4.7.1.1. Kuwaendeleza wale wanafunzi waliofanya vizuri na kuonesha maendeleo na hamu ya kazi fulani ya amali katika Elimu ya Sekondari ya Awali.

4.7.1.2. Kuwatayarisha vijana kumudu kazi walizojifunza na kuweza kuendelea na mafunzo ya juu zaidi ya fani walizochagua.

### 4.7.2. Sekondari Ya Jumla

Serikali itaendeleza baadhi ya skuli za sekondari kuwa ni sekondari za kawaida kulingana na mahitaji ya uchumi wa Taifa na kwa kuzingatia uwezo wa Serikali. Skuli za sekondari za kawaida zitawapa fursa ya kuendelea na masomo wanafunzi wa skuli za Sekondari ya Awali walioweza kufikia viwango vya kuingilia skuli hizo. Wanafunzi hawa watakuwa ni tofauti na wale watakaochaguliwa kujiunga na skuli za Sekondari za Michepuo ingawa nao watagawika katika nyanja ndogo ndogo za Sayansi, Lugha, Sayansi jamii n.k. Malengo ya sehemu hii yatakuwa:-

4.7.2.1. Kuwapa wanafunzi misingi ya sayansi na teknolojia pamoja na maarifa na stadi za sanaa na sayansi ya jamii zikiwemo kazi za utawala.

4.7.2.2. Kuwafanya wanafunzi watambue, waheshimu na watekeleze vizuri wajibu wao kwa Taifa.

4.7.2.3. Kujenga miongoni mwa wanafunzi tabia ya udadisi, uchunguzi, ugunduzi na ubunifu.

4.7.2.4. Kuyaendeleza mafunzo mbali mbali yaliyoanza katika skuli za Sekondari ya Awali kwa upana zaidi.

4.7.2.5. Kuwatayarisha wanafunzi ili waweze kumudu mafunzo ya ngazi za elimu ya juu kwa wale watakaoendelea.

## 4.8. ELIMU YA SEKONDARI YA JUU

Ni kiungo kizuri baina ya ngazi zote za elimu kabla na za baadaye. Kwa hivyo, ngazi hii ya elimu itawazingatia wale waliojitokeza na watakaokubalika kuwa watamudu vyema elimu ya ngazi za juu zaidi. Ngazi hii ya elimu itakuwa na madhumuni makuu ya kutayarisha wataalamu wa ngazi na aina mbali mbali na itagawika katika sehemu zifuatazo:- Sekondari ya Michepuo, Sekondari ya Juu ya Jumla.

### 4.8.1. Sekondari Ya Juu Ya Michepuo

Serikali itaanzisha na kuendeleza skuli za Sekondari za Michepuo kulingana na mahitaji ya Taifa na uwezo utavyokuwa. Michepuo itakayokuwepo katika Sekondari ya Juu italingana na michepuo ya Sekondari yaPili. Malengo ya ngazi hii ni:-

4.8.1.1. Kuwaendeleza wale wanafunzi waliofanya vizuri, walioonesha mwelekeo na hamu ya kazi fulani na waliofikia viwango vilivyowekwa.

4.8.1.2. Kuwapa wanafunzi fursa ya kujiendeleza zaidi katika fani walizozichagua.

4.8.1.3. Kutayarisha vijana kumudu vizuri zaidi kazi walizojifunza na kuendelea na mafunzo ya juu zaidi ya fani walizozichagua.

4.8.1.4. Kuwawezesha kukabili maisha kwa kujitegemea wenyewe.

**4.8.2. Sekondari Ya Juu Ya Jumla**

Serikali itaendeleza skuli za sekondari ya juu za elimu ya jumla kulingana na mahitaji ya uchumi wa Taifa na kwa kuzingatia uwezo wa Serikali. Malengo ya ngazi hii yatakuwa:-

4.8.2.1. Kuwaendeleza wanafunzi katika mafunzo kwa mujibu wa walivyofaulu.

4.8.2.2. Kuwawezesha wanafunzi kutekeleza vizuri zaidi majukumu yao na kukabili maisha ya baadae.

4.8.2.3. Kuwatayarisha wanafunzi kuonesha uwezo wa kumudu masomo kwa ajili ya masomo ya juu.

**4.9. ELIMU YA WALEMAVU**

Ulemavu, kwa kadri itakavyowezekana, hautokua kikwazo wala sababu ya kumnyima mwanaadamu haki yake ya elimu. Kwa hivyo, Wizara ya Elimu kwa mashirikiano na vyombo vyengine vya Serikali na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, itahakikisha kwamba haki na fursa za elimu zinatolewa kwa walemavu kwa misingi sawa na ile itolewayo kwa Wazanzibari wengine.Elimu ya walemavu itahusika na mafunzo ya walemavu ndani na nje ya mfumo mzima wa elimu kama ilivyoelezwa katika mfumo huo. Madhumuni makubwa ya elimu hii ni kuwasaidia

walemavu kwa kuwapa mafunzo kamili yatakayowasaidia kuyamudu maisha yao vyema. Ili walemavu wasijione wao wako tofauti na watu wengine, Wizara ya Elimu itachukua kila juhudi kuhakikisha kwamba hawabaguliwi katika kupewa elimu. Pale itakapolazimika kutumika skuli tofauti kwa walemavu itafanyika hivyo, lakini mitaala itayofuatwa haitabadilishwa ila tu ikiwa kufanya hivyo ni kwa manufaa ya walemavu wenyewe.

## 4.10. ELIMU YA WATU WAZIMA

Elimu ya Watu Wazima itakuwa na madhumuni na malengo yafuatayo:-

4.10.1. Kuwazindua watu kuondokana na mazoea ya hali ya maisha waliyokuwa wakiishi siku za nyuma na ambayo yaliwacheleweshа katika kuleta maendeleo yao.

4.10.2. Kuwapa wananchi misingi ya kujiendeleza hadi wafike kiwango cha juu cha uwezo wao wa kielimu, chini ya msingi wa Azimio la Kimataifa la Elimu Kwa Wote.

4.10.3. Kuwawezesha watu katika kila familia na/au kijiji, kujifunza mbinu za kufanya maisha yao yawe bora zaidi kwa kutumia maarifa, stadi na mbinu za kisayansi na kiteknolojia na kuzalisha mali kwa kutumia vizuri mazingira yao.

4.10.4. Kuwaelekeza wananchi ili waelewe na watekeleze Sera za Taifa.

4.10.5. Kuwapa misingi ya kusoma na kuandika wale wasiojua hayo kwa lengo la kufuta kabisa ujinga wa kutojua kusoma na kuandika kwa haraka kama itakavyowezekana.

4.10.6. Kuwaelimisha wanakisomo kwamba wao ni sehemu kamili ya Taifa na wanawajibika kuendeleza Taifa kulingana na uwezo wa kiwango chao cha elimu, umri,

nafasi yao katika jamii pamoja na ujuzi wao.

## 4.11. ELIMU YA KUJIENDELEZA

Elimu ya kujiendeleza ina lengo la kuisaidia elimu ya kawaida (formal education) katika utoaji wa mafunzo mbali mbali. Elimu hii ni mbali na mpango wa mafunzo kazini (in-service training). Utoaji elimu ya kujiendeleza utalingana na nafasi, fursa, mbinu na vyombo vyengine kwa hao watakaojiendeleza au hata daraja za mahitaji ya wajuzi katika fani mbali mbali. Utoaji wa elimu ya kujiendeleza ni fursa, lakini jamii, Serikali na vyombo vyengine vitajaribu kila itakapowezekana kuwahamasisha wananchi kujiendeleza. Elimu ya kujiendeleza itakuwa na malengo yafuatayo:-

4.11.1. Kuwapa fursa wale wote ambao wanataka kujiendeleza ki-elimu na ambao kwa sababu fulani walikosa elimu ya lazima.

4.11.2. Kuwasaidia wale waliopata fursa za kawaida kukuza ujuzi wao ili waweze kufanya vizuri zaidi katika maisha yao.

4.11.3. Kuwahamasisha watu wote katika kujiendeleza kwa kupitia ngazi mbali mbali zilizowekwa.

## 4.12. ELIMU YA UALIMU

Walimu ndio watekelezaji muhimu wa malengo yote ya elimu kwa jumla na katika kila ngazi, kwa hivyo utayarishaji wa walimu ni jukumu muhimu katika kuyafikia malengo hayo. Ikiwa utayarishaji wa walimu utakuwa na kasoro, ufanisi wa malengo hayo utakuwa mdogo. Kwa hivyo malengo ya mafunzo ya ualimu yatakuwa kama yafuatavyo:-

4.12.1. Kuwapa wanafunzi wa ualimu misingi ya kutosha ya taaluma za elimu na za masomo ili kuwawezesha kujiendeleza kila mara na kuwafanya wawe na uwezo mkubwa katika masomo watakayofundisha.

4.12.2. Kuwapa misingi ya elimu wanafunzi wa ualimu itakayowawezesha kufanya utafiti ili kupata ufumbuzi wa matatizo mbali mbali katika jamii.

4.12.3. Kuwapa wanafunzi wa ualimu, maadili na utamaduni wa Taifa pamoja na kuwawezesha kutumia elimu katika fani mbali mbali za sanaa, sayansi za jamii, sayansi na teknolojia katika ngazi mbali mbali za elimu nchini.

4.12.4. Kuwapa wanafunzi wa ualimu falsafa, maadili ya jamii, saikolojia na maarifa ili kuwawezesha kufundisha vizuri, kukuza na kupanua upeo wa elimu ya jumla.

4.12.5. Kuwapa wanafunzi wa ualimu mbinu za kuwalea watoto watakaokabidhiwa na Taifa na kukuza miongoni mwa watoto hao uraia mwema na moyo wa kujitolea kwa manufaa ya jamii na kwa faida ya Taifa.

4.12.6. Kuwakuzia uwezo wa kujenga wanafunzi watakaokabidhiwa ili wawe na tabia na mtazamo wa kisiasa na kiitikadi unaotakiwa kitaifa.

4.12.7. Kuwaongezea kipaji cha kuwaelimisha watoto maana halisi ya dhana ya Ujamaa na Kujitegemea.

# SURA YA TANO

## 5.0. MITAALA YA ELIMU

### 5.1. MAANA YA MITAALA

Mitaala ni ufafanuzi wa jumla wa shughuli zote zinazotakiwa kufundishwa katika taasisi mbali mbali za elimu. Mitaala hutafsiri madhumuni na malengo na kubuni njia bora ambazo zinaweza kutekelezeka ili madhumuni na malengo hayo yafikiwe katika kiwango kinachoridhisha. Mitaala haikusanyi masomo peke yake, lakini huainisha mbinu na njia zinazofaa kusomeshea dhana na mawazo yanayotakiwa. Aidha, mitaala hujumuisha mbinu na njia za tathmini za mafunzo yanayotolewa. Kwa hivyo, kutunga mitaala inayofaa ni hatua muhimu na nzito inayohitaji utaalamu maalum.

### .2. UKUZAJI WA MITAALA NA UTAFITI WA ELIMU

.2.1. Chombo cha kitaifa kinachoshughulikia ukuzaji mitaala kitaendelezwa kwa kupatiwa wataalamu na vifaa kulingana na ukuaji wa utaalamu wenyewe na mahitaji yatakayokuwepo. Chombo hicho kitakusanya sehemu zinazolingana na kazi zifuatazo:-

.2.1.1. Kuendeleza mafunzo ya ualimu kazini.

2.1.2. Utayarishaji na ukuzaji mitaala.

2.1.3. Utungaji na uchapishaji wa vitabu na utayarishaji wa vielelezo vya kufundishia.

2.1.4. Utafiti wa elimu.

2.1.5. Kutunga na kufuatilia mitaala yote ya elimu.

5.2.1.6. Kushauri juu ya mitaala yote iliyotungwa kabla mitaala hiyo haijathibitishwa na Wizara ya Elimu.

5.2.1.7. Kufuatilia, kutathmini na kutoa maoni na mapendekezo juu ya masomo na mafunzo yote yanayotolewa katika ngazi yoyote au mahali popote palipotajwa katika Sera hii.

5.2.1.8. Kuishauri Wizara ya Elimu juu ya masomo ya kufundisha katika ngazi mbali mbali na kima na uzito wa kila somo.

5.2.1.9. Kuishauri Wizara ya Elimu katika upangaji wa viwango vya kupasi katika mitihani mbali mbali itakayotungwa, kusahihishwa na kuthibitishwa hapa Zanzibar.

## 5.3. MITAALA YA ELIMU KATIKA NGAZI MBALI MBALI

### 5.3.1. Elimu Ya Maandalizi

Wanafunzi watakaopewa elimu hiyo ni wale wenye umri wa baina ya miaka mitatu na sita. Mbinu kubwa ya ufundishaji wao ni kwa kutumia michezo, vitendo na nyimbo. Mafunzo yatatolewa katika nyanja zifuatazo:-

- Hisabati
- Kiswahili
- Dini
- Elimu ya Mazingira (Historia, Sayansi, Sanaa,Usafi, Mazingira na Mahusiano ya Kijamii)
- Siasa/Maarifa ya Jamii
- Michezo/Utamaduni
- Mengineyo yatayoamuliwa.

**5.3.2. Elimu Ya Msingi**

Elimu ya msingi itagawika katika sehemu tatu. Sehemu hizo zitapewa majina ya Seksheni I, II na III, kama ifuatavyo:

***5.3.2.1. Seksheni I (Darasa la I mpaka la III)***

Masomo yatagawika katika maeneo yafuatayo:-

- Kiswahili
- Kiingereza
- Hisabati
- Dini
- Siasa/Maarifa ya Jamii
- Elimu ya Mazingira (Historia, Sayansi, Sanaa, Usafi, Akhlaki, Mazingira, Mahusiano ya Kijamii, Jiografia n.k.)
- Michezo/Utamaduni
- Amali na Uchoraji/Chipukizi
- Mengineyo yatayoamuliwa.

***5.3.2.2. Seksheni II (Darasa la IV mpaka V)***

Masomo yatagawika katika maeneo yafuatayo:-

- Kiswahili
- Kiingereza
- Kiarabu
- Hisabati
- Sayansi/Uwiano

- Siasa/Maarifa ya Jamii
- Elimu ya jamii (Historia, Jiografia, Mazingira, Mahusiano ya Kijamii n.k.)
- Dini
- Amali na Sanaa/Chipukizi
- Utamaduni na Michezo/Maktaba
- Mengineyo yatayoamuliwa.

### 5.3.2.3. *Seksheni III (Darasa la VI mpaka VII)*

Masomo yatakuwa kama yaliyopo katika Seksheni ya pili isipokuwa katika darasa la Saba badala ya kuwepo somo la Elimu ya Jamii yatakuwepo yafuatayo:-

- Jiografia
- Historia.

### 5.3.3. **Elimu Ya Sekondari Ya Awali**

Wanafunzi watakaoingia katika ngazi hii watakuwa wanakaribia kufikia au hata kuzidi umri wa miaka 14.

Wanafunzi hapa wengi wao watakuwa wanajitayarisha kumaliza kiungo cha kuendelea na Sekondari ya Pili. Katika ngazi hiyo imekusudiwa kuwa wanafunzi watakaomaliza hapo wawe wamepata elimu itakayowasaidia kuendelea na masomo, au kuanza kufanya kazi kwa ajili ya maisha yao na kutoa mchango kwa taifa.

Kwa hivyo mitaala ya sehemu hii ya Sekondari itakusanya masomo yafuatayo:-

- Kiswahili.
- Kiingereza.
- Hisabati.
- Fizikia.
- Kemia.
- Elimu ya Viumbe (Bayolojia).
- Historia.
- Elimu ya Siasa/Maarifa ya Jamii.
- Jiografia.
- Mafunzo ya Amali, Sanaa na Teknolojia (MENA).
- Elimu ya Michezo/Utamaduni.
- Dini.
- Lugha ya Kigeni (Kiarabu, Kifaransa n.k.).
- Mengineyo yatayoamuliwa.

**5.3.4. Sekondari Za Pili Na Juu**

Mitaala ya elimu ya ngazi hii itabuniwa juu ya msingi wa Mpango wa Elimu na Amali (MENA) na kuthibitishwa na Wizara ya Elimu. Wanafunzi watakaoingia ngazi hii watapewa fursa ya kuchagua au kuchaguliwa masomo na mafunzo watakayoonekana kuyamudu ili mradi tu masharti ya msingi ya mitihani ya Baraza la Mitihani la Tanzania yanatimizwa. Masomo ya Siasa yataendelea katika ngazi zote za elimu.

### 5.3.5. Mpango Wa Elimu Na Amali

Kwa jumla, mitaala ya ngazi zote za Sekondari na Ualimu itaandaliwa chini ya misingi ya Mpango wa Elimu na Amali (MENA), ambao utafafanuliwa katika waraka maalum utaoandaliwa. MENA ndiyo kiini cha mabadiliko ya usomeshaji katika sekondari, na itatengewa kiasi cha 25% ya muda wa masomo katika ngazi ya Sekondari ya Awali. MENA siyo tu itaoanisha elimu na kazi, bali pia itajenga na kukuza ubunifu (creativity) miongoni mwa wanafunzi, kutoa uongozi wa kazi (vocational-guidance), teknolojia, mbinu za usanii (design techniques) na mawasiliano kwa njia ya michoro (graphic communication). Katika ngazi ya Sekondari ya Awali, kazi za amali zitatofautiana baina ya maskuli kulingana na mazingira ya pahala, lakini mafunzo ya msingi ya ufundi na teknolojia yatakuwa ya namna moja kwa wote. Katika ngazi ya Sekondari ya Pili na ya Juu mafunzo yatagawika katika michepuo ya biashara, kilimo, uvuvi, sayansi ya nyumbani na mingineyo itayoonekana inafaa kulingana na wakati. Elimu ya kawaida itaendelea kufundishwa ili kukidhi mahitaji ya jamii.

### 5.3.6. Elimu Ya Ualimu Wa Ulezi/Maandalizi

Wizara ya Elimu itaandaa utaratibu wa kuandaa walimu maalum wa ngazi ya ulezi na maandalizi. Kiwango cha elimu ya chini cha walimu wa ngazi hii kitakuwa Sekondari ya Awali. Mitaala ya mafunzo yao italingana na utaalamu wa kufundisha watoto wenye umri wa miaka minne hadi sita. Pamoja na hivyo mitaala ya elimu ya ualimu kwa ngazi hii itakusanya masomo ya msingi yafuatayo:-

5.3.6.1. Masomo yaliyopangwa kusomeshwa katika ngazi hii na mbinu za kufundishia masomo hayo.

5.3.6.2. Saikolojia, Falsafa ya Elimu na masomo mengine yatakayowasaidia wanafunzi wa ualimu kuwa walimu na walezi bora.

### 5.3.7. Elimu Ya Ualimu Wa Msingi Na Sekondari Ya Awali

Sera hii inaelekeza kwamba ifikapo mwaka 2000, Zanzibar iwe imekwishajitosheleza kwa mahitaji ya walimu katika ngazi hii. Walimu watakaosomesha ngazi hizi watahitajika kuwa na utaalamu wa masomo watayosomesha kwa kiwango kikubwa zaidi ya kile kilichomo katika masomo yenyewe kwa kila darasa. Kwa hivyo kiwango cha chini cha kuingilia mafunzo ya ualimu wa ngazi hizi kitawekwa kila baada ya muda kulingana na ukuaji wa elimu zenyewe na kupanda kwa mafunzo yanayokusudiwa kutolewa. Hata hivyo, kwa kuanzia, mwalimu wa skuli ya msingi atatarajiwa awe na elimu isiyopungua ya Sekondari ya Pili. Walimu wa Sekondari ya Awali watatakiwa wawe na elimu si chini ya Kidatu cha Sita (au inayolingana nayo) na kuwa na stashahada ya ualimu.

Kwenye ngazi hizi mitaala ya elimu ya Ualimu itakusanya nyanja zifuatazo:-

5.3.7.1. Masomo yote yatakayosomeshwa katika ngazi hizo pamoja na mbinu za kusomeshea masomo hayo.

5.3.7.2. Falsafa ya Elimu, Saikolojia na fani nyengine za elimu zinazohusika na kazi ya ualimu.

5.3.7.3. Misingi ya Uendeshaji na uongozi wa Elimu na Skuli.

5.3.7.4. Misingi ya huduma ya kwanza.

5.3.7.5. Mpango wa Elimu na Amali

**5.3.8. Elimu Ya Ualimu Wa Sekondari Za Pili na Juu**

Walimu watakaosomesha ngazi hizi watakuwa wale waliomaliza vyuo vikuu na kupata angalau shahada ya kwanza (au inayolingana nayo). Kwa walimu wa aina hiyo, mitaala ya elimu ya ualimu itakuwa ile inayofuatwa au itakayobuniwa na vyuo vikuu vinavyotoa mafunzo yenyewe.

**5.3.9. Walimu Wengine**

Walimu watakaofundisha walemavu, watu wazima na kuendeleza wengine watafuata mitaala itakayobuniwa kulingana na mahitaji yatakayokuwepo. Hata hivyo, mitaala hiyo haitokuwa tofauti na ile ya walimu wengine isipokuwa kuhusu mbinu za ufundishaji ambazo zitalingana na utaalamu na watu wenyewe.

**5.4. MITAALA YA ELIMU YA WATU WAZIMA**

**5.4.1. Kusoma, Kuandika Na Kuhesabu**

Mitaala ya uwanja huu itakuwa na stadi zote kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na maarifa msingi kuhusiana na mbinu za kisasa za kilimo, shughuli nyingine za uzalishaji mali.

**5.4.2. Kisomo cha Kujiendeleza**

Mitaala ya elimu ya watu wazima katika uwanja h itabuniwa kwa kuzingatia mahitaji ya vikundi vya wa wafuatao:-

5.4.2.1. Wale ambao hawakumaliza elimu ya lazima amb watahitaji kujiendeleza kitaalamu hadi kufikia kiwar cha juu zaidi cha elimu.

5.4.2.2. Wale ambao wamehitimu kisomo cha kusoma, kuandika na kuhesabu (K.K.K.) na ambao wataonyesha hamu ya kujipatia elimu ya skuli. Mitaala ya vikundi hivyo italingana na ile itakayofuatwa katika skuli.

### 5.4.3. Mafunzo Ya Amali

Mitaala ya mafunzo ya amali itakusudiwa hasa kwa wale watakaomaliza vyema hatua zitakazotajwa katika K.K.K. Miongoni mwa amali zitakazopewa umbele ni zile ambazo zitasaidia kufanya maisha ya watu kuwa bora kadiri utaalamu wa amali zenyewe utavyoongezeka. Mkazo utawekwa katika kutunga mitaala ya kilimo, uvuvi, ufugaji, sayansi ya nyumbani na ufundi wa aina zote.

## 5.5. LUGHA ZA KUFUNDISHA NA KUFUNDISHIA

### 5.5.1. Lugha zitakazofundishwa

Kiswahili kitaendelea kusomeshwa kama somo peke yake na la lazima katika ngazi mbali mbali kama itavyoainishwa katika mitaala inayofuatwa. Pia lugha za Kiingereza na Kiarabu zitaendelea kusomeshwa kama masomo. Aidha, Wizara ya Elimu itazingatia uwezekano wa kusomesha lugha nyengine za kigeni kulingana na mahitaji yatakayokuwepo.

### 5.5.2. Lugha ZA Kufundishia

Kiingereza kitaendelea kuwa lugha ya kusomeshea kwa masomo yote katika Elimu ya Sekondari isipokuwa ya Lugha na Dini. Wakati huo huo Wizara ya Elimu itachukua juhudi katika kujiandaa kwa matumizi ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika elimu ya Sekondari siku za baadae, jamii itapohitaji na mazingira ya kiuchumi na kijamii kuruhusu.

**5.6. UKAGUZI WA ELIMU**

5.6.1. Kwa kuelewa kwamba shughuli za elimu katika ngazi zote haziwezi kwenda vizuri bila ya kuwa na usimamizi na ukaguzi mzuri, Wizara ya Elimu itaunda chombo maalum kitachosimamia shughuli za ukaguzi wa elimu katika ngazi zote isipokuwa elimu ya Chuo Kikuu. Chombo hicho kitakuwa na hadhi ya juu zaidi kuliko Idara zitakazokaguliwa na kitakuwa pia na uwezo wa kuzikagua skuli za watu binafsi. Pamoja na kazi nyengine, chombo hicho kitakuwa na majukumu yafuatayo:-

5.6.1.1. Kuhakikisha kwamba shughuli za elimu katika kila ngazi zinaendeshwa kama ilivyokusudiwa.

5.6.1.2. Kuhakikisha kwamba ngazi zote za elimu zinapatiwa walimu wa kutosha na wenye sifa za kusomesha ngazi hizo.

5.6.1.3. Kufuatilia usomeshaji katika ngazi zote na kutoa ushauri na maelekezo yanayofaa kwa walimu hao.

5.6.1.4. Kuijulisha Wizara ya Elimu juu ya matatizo na mafanikio ya sekta ya elimu na kushauri ipasavyo.

5.6.1.5. Kuijulisha Wizara ya Elimu juu ya hali ya majengo, samani, vifaa vya kufundishia, usafi wa mazingira na shughuli nyenginezo zinazofanyika katika maskuli.

**5.6.2. Maslahi Ya Mkaguzi**

Kwa kutambua kwamba Mkaguzi ana wajibu mkubwa wa kusimamia na kudhibiti elimu mashuleni, maslahi ya wakaguzi yatapewa mitazamo maalum kulingana na uzito wa kazi zenyewe, kama yatavyofafanuliwa katika muundo wa utumishi wa walimu, na nyaraka nyengine za Serikali.

# SURA YA SITA

## 6.0. WALIMU

### 6.1. MAANDALIZI YA WALIMU

Ili Sera hii ya Elimu itekelezwe kwa ufanisi unaotarajiwa itabidi walimu waandaliwe vizuri. Katika maandalizi hayo ubora na wingi wa walimu hao utazingatia mahitaji, lengo likiwa ni kujitosheleza ifikapo mwaka 2000.. Kwa jumla utaratibu wa kiasi cha walimu watakaoajiriwa utakuwa kama ifuatavyo:-

#### 6.1.1. Elimu Ya Msingi

Walimu 4 kwa kila madarasa matatu (3). Kila madarasa matatu, zaidi ya kuwepo walimu wanne atakuwepo mwalimu mmoja kwa kila somo lenye kuhitaji elimu na ujuzi maalum, kwa mfano, Kiarabu na Dini, Muziki, n.k.

#### 6.1.2. Elimu Ya Sekondari

Kwa sababu walimu katika ngazi hii ya elimu huwa na elimu ya ujuzi maalum wa somo/masomo, kila mwalimu atatarajiwa asomeshe vipindi visivyopungua 24 na visivyozidi 28, kwa wiki.

## 6.2. WAJIBU, HAKI, HUDUMA NA MASLAHI KWA WALIMU

### 6.2.1. Wajibu Wa Walimu

Kisheria wajibu wa mwalimu unaelezwa vyema katika Sheria ya Elimu. Aidha katika upangaji wa mitaala na usomeshaji kuna mategemeo ambayo hayatajwi wazi wazi katika sheria hiyo. Hata hivyo, mategemeo hayo huathiri kazi ya ualimu pale yasipokuwapo. Mbali na wajibu wake wa kuwafunza na kuwalea watoto wa Taifa hili kwa misingi inayokubalika, mwalimu pia ana wajibu ufuatao;-

6.2.1.1. Kuwaarifu wazazi dhamira za masomo na matendo ya skuli kabla na baada ya kubuni na kutekeleza mipango inayohusu skuli.

6.2.1.2. Kuwashauri wazazi juu ya mipango hiyo na kuwahusisha ili waweze kuunga mkono.

6.2.1.3. Kuwaarifu wazazi mara kwa mara kuhusu maendeleo ya watoto wao.

6.2.1.4. Kufahamu na kujaribu kukidhi haja za wanafunzi.

6.2.1.5. Kutumia njia bora zinazoweza kuvinyanyua viwango vyao vya usomeshaji.

6.2.1.6. Kukubali kuwa wao ni sehemu ya Taifa na kwa hivyo inawalazimu kuielewa vyema siasa ya nchi na sera za elimu ili waweze kuzifuata na kuzieleza kwa usahihi kwa wanafunzi wao.

6.2.1.7. Kuelewa majukumu yao kama yanavyoainishwa na kuelezwa katika Sheria na Kanuni za Elimu.

6.2.1.8. Kuelewa na kutekeleza kwa fikra na vitendo miiko ya kazi ya ualimu kama ilivyooneshwa katika Sheria na Kanuni za Elimu kwa mujibu wa miongozo ya Wizara ya Elimu inayotoka kila mara.

6.2.1.9. Kutumia nyenzo zinazopatikana katika mazingira yao kwa kuwapa ujuzi wa kujifunza wanafunzi wao bila ya

kuathirika sana na upungufu wa vifaa kutoka nchi za nje unapotokezea.

6.2.1.10. Kuinyanyua hadhi ya skuli katika jamii.

6.2.1.11. Kuzichukulia hatua ipasavyo sifa au lawama zitakazotolewa.

6.2.1.12. Kuinyanyua na kuilinda hadhi ya kazi ya ualimu.

**6.2.2. Haki Za Walimu**

Walimu kama wafanyakazi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wana wajibu wa kuzijua na kutimiziwa haki zao kama zinavyoainishwa katika Kanuni za Utumishi (General Orders), na matoleo mengine ya Serikali.

**6.2.3. Maslahi Ya Walimu**

Kutokana na umbile la kazi ya ualimu pamoja na tabia na sifa ambazo mtu anayekuwa mwalimu anahitajika kuwa nazo, Serikali itaweka ngazi maalum za mishahara badala ya zile zinazotumiwa katika muundo wa utumishi wa wafanyakazi Serikalini. Daraja za mishahara katika muundo huu zitatokana na kima cha elimu, muda wa mafunzo ya ualimu na uzoefu na uhodari katika kazi ya ualimu kwa mwalimu muhusika. Aidha wadhifa wa mwalimu aliyekwishasomea utaanza kutambuliwa tangu pale anapoingia kazini. Zitakuwepo daraja kuu zifuatazo za ualimu ambazo maslahi na masharti yake yatafafanuliwa katika Muundo wa Utumishi wa Walimu utaoandaliwa:-

| DARAJA YA UALIMU | SIFA |
|---|---|
| Mwalimu Daraja la IIIC | Elimu ya Sekondari ya Awali au ya Pili bila Mafunzo ya Ualimu |
| Mwalimu Daraja la IIIB | Elimu ya Sekondari ya Awali na Mafunzo ya Ualimu, au kupanda Daraja kwa IIIC. |
| Mwalimu Daraja la IIIA | Elimu ya Sekondari ya Pili na Mafunzo ya Ualimu, au Elimu ya Sekondari ya Pili, au kupanda Daraja kwa IIIB. |
| Mwalimu Daraja la IID | Stashahada ya Ualimu, au kupanda Daraja kwa IIIA. |
| Mwalimu Daraja la IIC | Shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu, au kupanda Daraja kwa IID. |
| Mwalimu Daraja la IIB | Shahada ya kwanza ya Uhandisi, au kupanda Daraja kwa IIC. |
| Mwalimu Daraja la IIA | Kupanda daraja kwa IIB. |
| Mwalimu Daraja la IC | Kupanda Daraja kwa IIA |
| Mwalimu Daraja la IB | Kupanda Daraja kwa IC |
| Mwalimu Daraja la IA | Kupanda Daraja kwa IB. |

### 6.2.4. Namna Ya Kuingia Na Kupanda kwa Walimu

Kama ilivyo katika uingizaji wa wafanyakazi Serikalini katika daraja mbali mbali watakuwepo walimu watakaoajiriwa moja kwa moja kutokana na sifa walionazo na vile vile walimu watakaoingia katika daraja kwa kupandishwa cheo baada ya kuonesha uwezo kati ya wengine, au kwa kupata mafunzo katika daraja hiyo.

Kutakuwapo kima cha muda usiopungua miaka fulani wa uzoefu kutegemea daraja yenyewe. Maelezo kamili ya kila daraja yatachambuliwa katika muundo wa utumishi wa walimu utaoandaliwa.

### 6.2.5. Walimu Waandamizi

Kutokana na wingi wa wafanyakazi/walimu ambao wana sifa na uzoefu unaolingana, haitawezekana kabisa kuwapatia nyadhifa wote, hata kama sifa za kuteuliwa katika nafasi hizo watakuwa nazo. Kwa hivyo, patakuwapo na nafasi maalum za nyadhifa zitazojulikana kama: "Walimu Waandamizi". Nyadhifa hizi zitakuwa kama Ualimu Mkuu au nyadhifa nyengine zozote, lakini hazitakuwa na dhamana za kiutawala. Hata hivyo, ukosefu wa dhamana za kiutawala hautaathiri mazingatio ya uwezo wa kusomesha au kufanya kazi nyengine yoyote ya kitaalamu katika uwanja wa elimu, na hivyo mshahara wa Mwalimu Mwandamizi utaweza kuwa mkubwa zaidi kuliko ule wa Mwalimu Mkuu au Afisa mwengine anaegezewa nae. Utaratibu huu utasaidia kuwapa motisha walimu wazuri wenye vipaji vya juu wanojituma, bila ya kulazimika kuwaondoa madarasani.

### 6.2.6. Huduma Maalum Kwa Walimu

Walimu ndio watekelezaji wakubwa wa Sera hii ya Elimu. Kwa hivyo, itahakikishwa kwamba pamoja na walimu kutimiziwa haki zao, watapatiwa huduma maalumu kwa mujibu wa masharti yatayoandaliwa kwa lengo la kuwapa motisha. Miongoni mwa huduma hizo ni kama zifuatazo:

6.2.6.1. Kwa madhumuni ya kuwatia moyo walimu ili wajiendeleze kimasomo, utabuniwa utaratibu wa kumrejeshea mwalimu aliyejiendeleza ada za kufanyia mitihani aliyojigharimia ikiwa atafaulu. Aidha, mwalimu

aliyejiendeleza atapatiwa nyongeza za mshahara na kupandishwa daraja kwa mujibu wa taratibu zitazowekwa.

6.2.6.2. Utawekwa mpango na masharti ya kuwakopesha walimu vipando (baiskeli, pikipiki n.k.) kwa lengo la kuwasaidia usafiri na utekelezaji mzuri wa kazi. Aidha, watapatiwa posho za usafiri kwa kadri itavyowezekana.

6.2.6.3. Posho maalum ya mazingira magumu itatolewa kwa wale walimu watakaofanya kazi katika skuli zenye shida kubwa kwa kadri ya Wizara ya Elimu itakavyoainisha, na kwa wale wataotakiwa kuchukua vipindi katika ngazi za juu ya zile wanazostahiki.

6.2.6.4. Utaandaliwa utaratibu utaohakikisha kwamba wakati wote kuna fursa za mafunzo ya ualimu kazini yatayotolewa kwa njia mbali mbali k.v. semina, warsha, ziara za mafunzo na mafunzo maalum yatayotolewa katika vituo (residential training), na nje ya vituo (distance educational training).

6.2.6.5. Kwa kuzingatia kwamba walimu wanafanya kazi zao vizuri zaidi ikiwa wanaishi karibu na skuli wanazosomesha, Wizara ya Elimu itawahamasisha na kushirikiana na wananchi katika kuwajengea walimu nyumba zao kwa mujibu wa taratibu zitazowekwa.

6.2.6.6. Itatolewa posho maalum ya usomeshaji (teaching allowance) kwa walimu wote watakaokuwa wanasomesha madarasani, na wengine wataoainishwa kila mara katika matoleo ya kiserikali. Pia kutakua na posho za dhamana kwa nyadhifa za uongozi wa elimu zitakazoainishwa katika matoleo.

### 6.2.7. Mafunzo Ya Uongozi Wa Elimu

Utaratibu mahsusi unaoeleweka utaandaliwa utaohakikisha kwamba wote wanaoteuliwa katika nyadhifa mbali mbali za uongozi wa elimu, wanapatiwa

mafunzo yanayohusiana na nyadhifa zao.

Utaratibu huo utajumuisha uanzishaji wa kozi maalum za uongozi katika Chuo Cha Ualimu cha Nkrumah na vyenginevyo vitavyoanzishwa, na matumizi ya fursa zilizoko Tanzania Bara na nje ya Tanzania.

# SURA YA SABA

## 7.0. UONGOZI WA ELIMU

### 7.1. WIZARA NA VIONGOZI WA ELIMU

Sera hii ni ya elimu na kwa hivyo sehemu kubwa ya utekelezaji wake itategemea ubora wa Wizara ya Elimu. Hivyo ili utekelezaji huo uwe wa kiwango kikubwa cha mafanikio itahitaji uteuzi wa viongozi mbali mbali ufanywe kwa kuzingatia uzoefu, ujuzi, maarifa na uhodari wa viongozi hao.

### 7.2. UTEUZI WA VIONGOZI WA ELIMU

#### 7.2.1. Viongozi Wa Ngazi Za Juu

Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Maafisa wengine wenye nyadhifa kama hizi ambazo Serikali itaona ipo haja ya kuwepo, watateuliwa na Rais wa Zanzibar.

#### 7.2.2. Viongozi Wa Ngazi Za Kati

Wakuu wa Vitengo, Sehemu, Sehemu ndogo, Walimu Wakuu, Wakaguzi wa elimu na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya watateuliwa na Waziri wa Elimu kwa mujibu wa sheria zitazowekwa. Maafisa wengine watateuliwa na Tume ya Uajiri wa Walimu kwa kushauriana na Wizara ya Elimu. Uteuzi wa viongozi wa ngazi mbali mbali kwa kuzingatia sifa zitakazowekwa utaoanishwa na maslahi na marupurupu kama yatakavyopangwa.

7.2.3. **Viongozi Wa Ngazi Za Chini (Maafisa Wasaidizi - Desk Officers)**

Watateuliwa na Wizara ya Elimu.

7.2.4. **Viongozi Wa Muda**

Utabuniwa utaratibu wa kuteua kiongozi wa muda kwa wadhifa utakaokosa afisa mwenye sifa zitazowekwa. Kiongozi huyo atatambuliwa kwa kupewa posho la muda la kukaimu kwa mujibu wa kanuni za kazi (General Orders) zitakazokuwepo wakati huo.

## 7.3. MUUNDO WA UONGOZI WA ELIMU

Wizara ya Elimu itaendelea kuwa chombo cha Taifa la Zanzibar kinachoratibu, kusimamia na kuendesha sehemu kubwa ya huduma za elimu. Muundo wake utalingana na aina za elimu pamoja na maendeleo ya elimu na jamii yatakayotokea.

## 7.4. WAJIBU WA WIZARA YA ELIMU

Wizara ya Elimu kwa kutumia muundo wake wa uendeshaji na viongozi wake italazimika kutumia nyenzo itakazokuwa nazo kwa madhumuni ya kuzisaidia taasisi zote za elimu zitakazokuwepo nchini ili ziweze kutoa huduma bora za elimu kwa Wazanzibari. Katika kuyatimiza hayoWizara ya Elimu itawajibika ifuatavyo:

7.4.1. Kuendeleza na wakati mwingine kushauri kuifanyia marekebisho Sera na Sheria ya Elimu ili kuziwezesha taasisi za elimu zitakazokuwepo kufanya kazi ya kutoa huduma za elimu ipasavyo.

7.4.2. Kuiendeleza na kurekebisha miongozo na mipango ya mitaala, utekelezaji wake na mipango ya skuli.

7.4.3. Kupendekeza mipango itayofaa katika kunyanyua viwango vya elimu nchini.

7.4.4. Kuendeleza na kuzipatia skuli na vyuo mihutasari, miongozo ya kusomeshea na vifaa vyengine vinavyohitajika kufundishia wanafunzi.

7.4.5. Kuzitumia ipasavyo nyenzo (watu, fedha na vifaa) zitakazokuwepo.

7.4.6. Kuthbitisha na kuendeleza mihutasari.

7.4.7. Kuarifu jamii juu ya hali ya elimu nchini, na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi zote za elimu nchini.

7.4.8. Kutoa miongozo ya kisera, kusimamia na kuratibu shughuli zote za kielimu za taasisi zote za kiserikali na zisizokuwa za kiserikali zinazotoa aina zote za elimu nchini.

## 7.5. AFISI ZA ELIMU ZA MIKOA NA WILAYA

Kufuatia Sera ya madaraka Mikoani, Wizara ya Elimu itazlimarisha Afisi za elimu za Mikoa na Wilaya ili kusimamia kwa ufanisi zaidi uendeshaji wa shughuli zote za elimu katika Mikoa na wilaya. Kwa vile Afisa wa Elimu wa Mkoa/Wilaya ndiye msimamizi mkuu wa utekelezaji wa shughuli za elimu katika Mkoa/Wilaya uteuzi wake utatokana na sifa maalum zitazowekwa. Aidha maslahi na marupurupu maalum yatawekwa kwa afisa huyo kulingana na uzito wa dhamana yake.

## 7.6. SKULI NA WAJIBU WAKE

7.6.1. Skuli ni taasisi muhimu zilizopangwa kutoa elimu ya desturi (formal education). Kwa vile taasisi hizo hutarajiwa kubuni na kutekeleza ufafanuzi wa madhumuni na malengo ya elimu kufikia kiwango kinachoridhisha, ni muhimu malengo ya skuli

yaainishwe kwa uwazi, kama ifuatavyo:-

7.6.1.1. Kuendeleza miongoni mwa wanafunzi, akili zenye tabia ya kuchunguza mambo, kupenda kujifunza na kuwa na tabia ya kukubali kutumia uwezo wao kwa kazi zenye manufaa.

7.6.1.2. Kuimarisha na kuendeleza uwezo wa wanafunzi wa kufikiria njia zilizo bora za kuleta maendeleo yao na Taifa.

7.6.1.3. Kudumisha imani ya kuheshimu, kujiheshimu na kuthamini wengine.

7.6.1.4. Kuendeleza moyo wa kujishirikisha katika mambo yenye faida kwa mtu binafsi na jamii kwa jumla.

7.6.1.5. Kuanzisha, kuimarisha na kuendeleza stadi za kutoa ushauri na kutafuta ufumbuzi wa matatizo.

7.6.1.6. Kujielewa na kuuelewa ulimwengu.

7.6.1.7. Kuwa na uwezo wa kutumia stadi zifaazo katika maisha ya utu uzima na maisha ya kuajiriwa kazini au ya kujiajiri mwenyewe.

# SURA YA NANE

## 8.0. VYOMBO VINGINE VYA ELIMU

### 8.1. VYOMBO NA TAASISI ZA ELIMU

Zaidi ya kuwepo Wizara ya Elimu kwa muund ulliokwishaelezwa, kutakuwa na vyombo na taasisi z elimu ambazo zitapewa hadhi na uzito wa kisheri Aidha kutakuwepo na vyombo vitakavyotamkwa katik Sheria ya Elimu, ambavyo vitakuwa na madhumur ya kuwashirikisha wazazi na taasisi mbali mbali z Serikali katika kuongoza na kuendeleza elimu - kw mfano; Baraza la Elimu, Bodi ya Elimu ya Juu, Bodi z Elimu za Mikoa na Wilaya, Kamati za Maskuli n.k.

### 8.2. TAASISI YA LUGHA

Serikali ya Mapinduzi imeanzisha Taasisi ya Kiswahi na Lugha za Kigeni kwa lengo kubwa la kukuza n kukiendeleza Kiswahili pamoja na kufundisha lugh za kigeni kwa wananchi na Kiswahili kwa wageni.Ser kuu inayoambatana na kuanzishwa kwa Taasisi h inatokana na haja ya kusomesha Kiswahili cheny kiwango kikubwa na mfano katika usahihi wake kw sababu Zanzibar ina historia kubwa ya Kiswahili. Pi Taasisi itakuwa chombo cha kuhimiza kufunzwa lugh za kigeni kwa kiwango hicho chicho.

### 8.3. MAKTABA

Maendeleo katika sekta zake zote hutegemea sana ujuzi uwezo na maarifa waliyonayo watenda kazi katika sekt na ngazi mbali mbali. Ili watenda kazi hao wawez kuendeleza ujuzi, uwezo na maarifa hayo, ni lazim wapate fursa ya kujiendeleza kwa kupata ushauri w

kitaalamu unaohusiana na fani za kazi zao.

Mojawapo ya njia za kupata hayo ni kwa kupitia maandiko mbali mbali. Maktaba ni miongoni mwa pahala ambapo maandiko mbali mbali yanapatikana kwa madhumuni ya kuwasaidia wataalamu na watu wengine kujifunza mambo mbali mbali. Kutokana na umuhimu wa maktaba kwa maendeleo ya Taifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaunda Taasisi ambayo itasimamia na kuratibu shughuli zote za maktaba nchini.

## 3.4. MAKTABA KUU

Kwa kutambua umuhimu wa maktaba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itachukua juhudi ya kuanzisha Maktaba Kuu. Zaidi ya madhumuni ya maktaba hiyo yaliyoelezwa hapo juu, pia maktaba yenyewe itakuwa ni mahali pa kupata kumbukumbu mbali mbali, chimbuko la utafiti, mafunzo kwa wakutubi na kuzihudumia maktaba nyengine zitakazokuwepo.

## 3.5. MAKTABA ZA WILAYA

Wizara ya Elimu itahimiza na kushawishi uanzishaji wa maktaba za wilaya. Serikali za Wilaya nazo zitashawishiwa kuanzisha maktaba za maeneo zitazoendeshwa na Serikali za Mitaa.

## 3.6. MAKTABA ZA SKULI

Wizara ya Elimu itahimiza na kutoa msukumo kwa maskuli ili yajenge utamaduni wa kuanzisha, kutunza na kuendesha maktaba za skuli na hata za madarasa. Kifungu maalumu cha fedha kitatengwa kwa ajili hii katika Wizara ya Elimu.

**8.7. TUME YA UTUMISHI WA WALIMU**

Itaundwa Tume ya Utumishi wa walimu yenye ngu\ za kisheria itayoshughulikia ajira, huduma, wajib haki na maslahi ya walimu.

**8.8. TAASISI ZA MAFUNZO YA UFUNDI STAI (VOCATIONAL TRAINING)**

MENA haitoshi kuwaandaa kikamilifu vijana wot wanaomaliza skuli katika hatua mbali mbali, kwa ka za kuajiriwa au kujiajiri wenyewe. Hii ni kutokana n ukweli kwamba, kwa vyo vyote vile, skuli haziwe kufundisha amali (skills) zilizokamilika, kwani hayo siy madhumuni ya msingi ya skuli. Mazingira ya skul yanatofautiana sana na hali halisi ya mazingira ya kazi Ni dhahiri, na mafunzo ya amali yanayotolewa skul hayawezi kukidhi moja kwa moja mahitaji ya sehemu za kazi. Kwa hivyo, kwa kadri mafunzo ya amal yatavyotolewa skuli, hayawezi kukamilisha ujuzi wa amali, bali yanasaidia tu kumpa mwelekeo kijana katika amali fulani ili aweze kuanza kuitumia inapobidi, na muhimu zaidi aweze kufunzika kwa urahisi zaidi hap baadae katika amali hiyo. Hapo ndipo unapojitokeza umuhimu wa taasisi za mafunzo ya ufundi stadi. Taasis hizi zinaweza kuwa za kiserikali au za watu binafsi, na zinaweza kutoa mafunzo rasmi (formal training) au yasiyo rasmi (in-formal training). Utaratibu na mashart ya utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi nchin yatatandikwa katika sera maalum ya kitaifa ya utoaj wa mafunzo hayo itayoandaliwa na chombo cha Serikal ya Mapinduzi ya Zanzibar kinachoshughulikia mamb ya kazi au chenginecho chochote kinachohusika Miongoni mwa mengi mengine, sera hiyo itaelekez utaratibu utaovifanya viwanda na taasisi nyengin zinazoajiri, zishiriki kikamilifu katika kugharimi mafunzo ya ufundi stadi.

# SURA YA TISA

## 9.0. MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA SERA HII

### 9.1. MALIPO YA USAFIRI KWA WANAFUNZI

Mashirika ya usafiri na vyombo vya binafsi vya usafiri vitakavyokuwepo vitatakiwa kufuata utaratibu wa usafiri duniani wa kulipisha wanafunzi nauli nafuu. Utaratibu huu wa nauli nafuu utatumika kwa wale wanafunzi wenye uthibitisho wa Wizara ya Elimu na/ au Chuo kinachohusika.

### 9.2. BARAZA LA MITIHANI YA TAIFA LA TANZANIA

Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania litatunga mitihani maalum kwa ajili ya kutahini masomo ya MENA, na mengineyo ambayo yatakuwa yanatolewa Zanzibar tu bila ya kujali kama pia yanatolewa Tanzania Bara au la.

### 9.3. ELIMU KWA AJILI YA VYOMBO VYA HABARI

Zanzibar imebahatika kwa kuweza kuwa na nyenzo nyingi zinazoweza kutumika kwa kusomeshea kwa njia za kisasa. Kinachohitajika ni kuwepo kwa utaratibu bora na utaaalamu unaofaa. Kwa hivyo, Wizara ya Elimu itaanzisha mpango wa kushirikiana na Wizara inayosimamia vyombo vya habari kutumia njia ya kutoa elimu kwa wanafunzi na wananchi kwa redio, televisheni na magazeti. Vyombo vitakavyoshirikishwa katika mpango huu vitakuwa ni Idara ya Utafiti wa Elimu na Ukuzaji Mitaala, Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Idara ya Elimu ya Watu Wazima, Televisheni

Zanzibar, Sauti ya Tanzania, Zanzibar, Kituo cha Vielelezo kilichoko Chuo Cha Ualimu Nkrumah, na vyenginevyo vitavyoonekana vitasaidia. Aidha misaada kutoka kwa wahisani mbali mbali wa ndani na nje itatafutwa, katika kugharimia mipango itayoandaliwa ya utoaji wa elimu kwa vyombo vya habari.

## 9.4. MCHANGO WA WANANCHI KATIKA GHARAMA ZA ELIMU

Wizara ya Elimu itabuni mpango wa kuwa na kikosi cha kudumu cha ujenzi kitachopewa dhamana ya utengenezaji wa nyumba za walimu, majengo ya skuli na samani zinazohitajika. Katika ujenzi na utengenezaji huo, Wizara ya Elimu itazishirikisha Serikali za Mitaa na Kamati za Skuli katika kuwahamasisha wananchi kuchangia nguvu zao na vifaa vinavyopatikana vijijini. Aidha Wizara itakuwa ikiandaa mipango itayowawezesha wananchi kuchangia kwa njia ya kununua baadhi ya vifaa vya skuli ambapo kiasi kitachotumiwa kitahesabika kuwa ni mchango wa wananchi. Michango ya hiari ya moja kwa moja pia itahamasishwa kutoka kwa wananchi, makampuni na mashirika ya watu binafsi na ya Serikali.

Skuli za watu binafsi zitazotoza ada zitaruhusika katika ngazi za Elimu ya Maandalizi, Elimu ya Sekondari ya Pili na kuendelea, na mafunzo ya ufundi wa fani mbali mbali.

## 9.5. UTHIBITISHO WA VYETI VYA MASOMO

Wizara ya Elimu, kwa ushirikiano na vyombo vyengine vinavyohusika, itatathmini sifa na uzito wa cheti, stashahada au/na shahada na kukubali au kukataa au kutoa masharti au muda wa majaribio kwa vyeti hivyo vya elimu kuthibitishwa.

**9.6. HATUA ZA UTEKELEZAJI**

Sera hii baada ya kukubaliwa na Serikali itapangiwa programu za utekelezaji ambazo itazingatia kwa ukamilifu maelekezo ya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar, uwezo wa Taifa kwa jumla, na hisia za jamii katika kila hatua ya utekelezaji.

# SURA YA KUMI

## 10.0 MWISHO

10.1 Utekelezaji wa Sera hii ya Elimu, utatuhakikishia kudumishwa kwa misingi iliyowekwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, ambayo inahakikisha utoaji wa elimu kwa wote bila ya ubaguzi wa rangi, dini, kabila na mwengineo wowote, na bila ya kujali kipato cha mtu au hadhi yake katika jamii.Wakati misingi hiyo inadumishwa, Sera imetoa msukumo mkubwa wa kulifanya Taifa liende na wakati katika suala zima la utoaji elimu katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia, ikitoa nafasi kubwa ya kujifunza kwa wenzetu.

10.2 Aidha, utekelezaji wa Sera hii kwa ukamilifu utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza pengo liliopo baina ya elimu na ulimwengu wa kazi, kwa vile mpango wa MENA utakuwa umewaandaa vya kutosha vijana wanaomaliza skuli kwa ajili ya kazi za kuajiriwa na za kujiajiri wenyewe. Kama hatua hiyo itakuwa imefikiwa, basi tutakuwa tumefanikiwa kuyafikia malengo ya Elimu ya Kujitegemea.

10.3 Kwa jumla, kwa Sera hii ya Elimu, sasa tuna dira inayoeleweka na kukubalika ya kutufikisha tulikokusudia - yaani kujenga Taifa lenye usawa, lililoelimika, linalojitegemea kwa wataalamu wazalendo na ambalo litaweza kuishi kwa hadhi na heshima katika karne ya 21 inayojitokeza kwa kiwango cha juu kabisa cha teknolojia. Ili kufikia huko, kila Mzanzibari atawajibika kushiriki kikamilifu na kuchangia kwa hali na mali katika utekelezaji wa Sera hii. Hii ni changamoto yetu sote. Tujidhatiti kuikabili.

# NYARAKA MUHIMU ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAYARISHAJI WA SERA HII


1. Cambridge Education Consultants (1990); "An Examination of the Education Sector in Zanzibar" - a draft report prepared for The Ministry of Education, Zanzibar under Overseas Development Administration (ODA) Financial Support; Unpublished.

2. Chama Cha Mapinduzi (CCM) (1967); ":Azimio la Arusha", Kiwanda Cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA), Dar-es-Salaam.

3. Chama Cha Mapinduzi (CCM) (1987); "Program ya Chama Cha Mapinduzi 1987 - 2002", CCM - Dodoma.

4. Chama cha Mapinduzi (CCM) (1987); "Sera ya Malezi ya Taifa kwa Watoto na Vijana Tanzania", Dar-es-Salaam University Press.

5. Danish International Development Agency (DANIDA); "Identification on Study of Manpower Development and Training Needs in Zanzibar"; Draft Final Report Prepared by Cowiconsult, Unpublished.

6. Danish International Development Agency (DANIDA) (1990); "Identification of Technical Education Pilot Project in Zanzibar" - Interim Report Prepared by Cowiconsult - DANIDA Ref. No. 104 Tanzania/Zanzibar, Unpublished.

7. Goranson Ulf (1986), "Education in Zanzibar" - SIDA Education Division Documents No. 33 - Swedish Internatrional Development Authority (SIDA), Stockholm.

8. Karume, Abeid A. (19970); "Mabadiliko ya Elimu Zanzibar" - Hotuba ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume aliyowatolea walimu tarehe 21 Machi, 1970,

Katika Chuo Cha Lumumba - Shirika la Upigaji Chapa, Zanzibar.

9. Karume, Abeid A. (1971); Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi wote wa Zanzibar", Hotuba ya Marehemu Shekh Abeid Amani Karume ya tarehe 7/7/71; Shirika la Upigaji Chapa, Zanzibar.

10. Ministry of Education, Zanzibar, 'The Concept of Productive work in Schools (MENA) and Production Secondary School (PSS) in Zanzibar" - excerps from UNESCO's Integration of Education and Productive work in Zanzibar" - Unpublished.


11. Nyerere, J.K. (1967); "Azimio la Arusha" - katika "Ujamaa ni Imani 2" - Hotuba ya Mwalimu Julius K. Nyerere - juu ya Azimio la Arusha; East African Published House' Nairobi.

12. Nyerere J. K. (1967)' "Elimu ya Kujitegemea"; Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA) - Dar-es-Salaam.

13. Unesco (1982)' "Integration of Education and Productive Work in Zanzibar" - Serial No. ASMS/ED/EFP/014 - Paris.

MCHORO "A"

**MUUNDO WA MFUMO WA ELIMU WA ZANZIBAR**




**KIELELEZO:**

MTSA = Mtihani wa Taifa wa Sekondari ya Awali.
MOL = Mtihani wa 'O' Level.
MAL = Mtihani wa 'A' Level.
FTC = Full Technician Certificate.
MDL = Mtihani wa Diploma ya Lugha.
MCU = Mtihani wa Cheti cha Ualimu.
MDU = Mtihani wa Diploma ya Ualimu.
MDUF = Mtihani wa Diploma ya Ufundi.
MTT = Majaribio ya Trade Test.
EJ = Elimu ya Juu.
TKLK= Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni